



East African Journal of Swahili Studies

ejss.eanso.org

Volume 9, Issue 1, 2026

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana

Edward Ekadeli Lokidor^{1*}

¹ Chuo Kikuu kishirikishi cha Turkana, S.L.P. 69-30500, Lodwar, Kenya.

* Barua pepe ya mawasiliano: lokidorbalozi@gmail.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4667>

Tarehe ya Uchapishaji: **IKISIRI**

18 Machi 2026

Istilahi Muhimu:

Ufunzaji,
Ujifunzaji,
Lugha,
Elimu watu.

Makala hii inaeleza dhima ya Kiswahili katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji wa darasa la elimu ya watu wazima (Ngumbaru) katika kaunti ya Turkana. Data ya utafiti ilikusanywa nyanjani kupitia mahojiano na uchunzaji. Nadharia ya Kitamaduni ya Vygotsky ilielekeza uchanganuzi wa data. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba wanafunzi wa elimu ya watu katika kaunti ya Turkana wana ugumu wa kuelewa Kiingereza ambacho ni lugha ya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo yote isipokuwa Kiswahili. Kutokana na ugumu wa kuelewa Kiingereza walimu hulazimika kutumia Kiswahili ili kurahisisha uelewa wa matini katika kipindi darasani. Matokeo ya utafiti huu yataboresha kiwango cha elimu ya watu wazima na kupunguza idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika nchini Kenya.

APA CITATION

Lokidor, E. E. (2026). Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana; *East African Journal of Swahili Studies*, 9(1), 191-198. <https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4667>

CHICAGO CITATION

Lokidor, Edward Ekadeli 2026. "Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana". *East African Journal of Swahili Studies* 9 (1), 191-198. <https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4667>

HARVARD CITATION

Lokidor, E. E. (2026) "Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana", *East African Journal of Swahili Studies*, 9(1), pp. 191-198. doi: 10.37284/jammk.9.1.4667

IEEE CITATION

E. E., Lokidor "Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana ", *EAJSS*, vol. 9, no. 1, pp. 191-198, Mar. 2026.

MLA CITATION

Lokidor, Edward Ekadeli. "Dhima ya Kiswahili katika Elimu ya Watu Wazima katika Kaunti ya Turkana". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 9, no. 1, Mar. 2026, pp. 191-198, doi:10.37284/jammk.9.1.4667.

UTANGULIZI

Elimu ya watu wazima ilianzishwa nchini Kenya baada ya Kenya kupata uhuru kutoka ukoloni wa Uingereza (Bunyi, 1999). Lengo la kuanzishwa kwa elimu ya watu wazima lilikuwa kuwawezesha watu wazima kujua kusoma, kuandika, na kuhesabu. Wakati huo kulikuwa na idadi kubwa ya watu wasiojua kusoma na kuandika taifani. Kwa hivyo serikali ya Kenya ilianzisha elimu ya watu wazima ili kuwawezesha kujihusisha katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, kwa miaka ya hivi karibuni, elimu ya watu wazima imewapa watu wazima nafasi ya kupata elimu. Hii ni kwa sababu elimu ni kienzo muhimu cha kupata ajira au kujiunga na asasi za elimu ya juu.

Hata hivyo elimu ya watu wazima imekubwa na changamoto tele nchini Kenya tangu kuanzishwa. Mojawapo ya changamoto ni kuwa wanafunzi hawafanyi vyema katika mitihani ya kitaifa. Vilevile kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamewacha masomo kabla ya kufanya mitihani ya kitaifa (Gabriel na wengineo, 2016). Kwa wakati uo huo wanafunzi wa elimu ya watu wazima wanapata changamoto ya kuelewa masomo yanayofundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Hii ni kwa sababu hawakupata msingi thabiti wa kujifunza Kiingereza kama wanafunzi walio katika mfumo anuwai wa elimu. Hali imepelekea watu wazima kuamua kujiunga na shule za kawaida ili kufanya mitihani wa darasa la nane na mitihani wa kidato cha nne.

Licha ya changamoto hizi tele, tafiti chache ndizo ambazo zimeelekezwa kwa elimu ya watu wazima nchini Kenya. Kwa hivyo utafiti huu ulikusudia kuchunguza sababu za kutumia Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana.

Lugha ina nafasi muhimu katika mtalaa wa elimu ya taifa lolote lile hivi kwamba kupewa kipaumbele mbele katika mitalaa ya shule na vyuo vikuu mbalimbali duniani (Habwe na wenzake, 2010).

Nchini Kenya, Kiingereza na Kiswahili ni lugha za ujifunzaji na ufundishaji. Kiswahili ni lugha ya ujifunzaji na ufundishaji katika gredi la kwanza hadi la tatu ilhali Kiingereza ni lugha ya ujifunzaji na ujifunzaji masomo yote isipokuwa Kiswahili kuanzia gredi ya nne hadi vyuo vikuu (Lokidor, 2025; Habwe na wenzake, 2010). Kwa hivyo lugha ina nafasi ya kipekee katika mtalaa wa elimu kwa sababu hufanikisha mawasiliano darasani, kusahilisha uelewa wa matini na kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Hata hivyo, lugha huweza kuwa kizingiti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji matini darasani iwapo wanafunzi hawafahamu vyema lugha inayotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji darasani (Lokidor & Chimbutane, 2024). Vile vile Dixon (2018) anaeleza kwamba ufasaha wa lugha ni kigezo muhimu katika mtagusano na ujumuikaji wa jamii. Kwa hivyo, kutofahamu lugha nikizingiti cha mawasilianodarasani. Mawasiliano hufanikisha uelewa na umilisi wa maarifa, ujuzi na maadili yanayopitishwa katika elimu. Hii ina maana kwamba matumizi ya lugha wasiofahamu wanafunzi hutinga mawasiliano, hivyo basi wanafunzi kukosa kuelewa na kumaizi maarifa, ujuzi na maadili.

Watu wengi nchini Kenya wanafahamu Kiswahili kuliko Kiingereza. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya na kwa hivyo kutumiwa katika mawasiliano mapana katika shughuli mbali (Iribemwanga Mukhwana, 2011). Kwa upande mwingine wananchi wengi hawafahamu Kiingereza hasa wale ambao hawajapata kusoma. Kwa hivyo utafiti ulichunguza sababu za walimu na wanafunzi wa elimu ya watu wazima kutumia Kiswahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa masomo yanayofaa kufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza

NADHARIA YA VYGOTSKY YA KITAMADUNI

Nadharia hii iliasisiwa na Vygotsky mwaka wa 1980 ilitumiwa katika utafiti. Nadharia hii inatambua lugha kama stadi ambayo inaendelezwa katika muktadha wa utamaduni katika jamii. Pia nadharia hii inaeleza kuwa ujifunzaji lugha hutokea katika mazingira ya utamaduni wa jamii husika kwani lugha ni chombo cha utamaduni (Habwe na wengineo, 2010). Mihimili ya nadharia hii iliyotumika katika utafiti huu ni kuwa lugha ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Kwa hivyo nadharia hii iliniwezesha kubaini dhima ya Kiswahili katika ujifunzaji na ufundishaji masomo katika darasa la elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana. Pia nadharia hii inadai kuwa lugha huwezesha ushirikiano baina ya wanafunzi na walimu darasani. Mhimili huu ulitwezesha kubaini namna Kiswahili kinawawezesha wanafunzi kushiriki ipasavyo darasani. Hii ni kwa sababu lugha hutumiwa kujenga uhusiano na maingiliano ya watu katika shughuli mbalimbali kwa mfano shughuli ya elimu (Habwe na wenzake, 2010; IribeMwangi na Mukhwana, 2011). Vile vile nadharia hii ilitwezesha kubaini kwamba mwalimu hutumia lugha kuwasaidia wanafunzi kuelewa maarifa darasani (Habwe na wenzake, 2010). Hatimaye nadharia hii inaeleza kuwa maarifa na ujifunzaji hupatikana kutokana utangamano kati ya mtu na mazingira anamokulia. Kwa hivyo wanafunzi wa elimu ya watu wazima wanaelewa lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha inayowaleta Wakenya wengi pamoja taifani (IribeMwangi na Mukhwana 2011). Vilevile lugha ndiyo hutekeleza jukumu la kumlea na kumwelekeza mtoto kuelewa mazingira yake na kwa namna hiyo kukua kikamilifu (Habwe na wenzake, 2010).

METHODOLOJIA

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa kukusanya data katika mazingira halisi ya darasa la elimu ya watu

wazima katika kaunti ya Turkana. Data kutoka nyanjani na maktabani zilichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Aidha, mtafiti hakuwa na udhibiti juu ya watafitiwa katika darasa la elimu ya watu katika kaunti ya Turkana.

Njia za Utafiti

Utafiti huu ulitumia uchunzaji, mahojiano na uchanganuzi wa matini kukusanya data.

Mahojiano

Mahojiano yalenga walimu na wanafunzi wa elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana. Kabla ya kuanza mahojiano wahusika walielezwa kuhusu lengo la utafiti na kuomba idhini yao kushiriki kwa kutia sahihi kwenye fomo ya dhamiri. Niliwahoji wanafunzi wa elimu ya watu wazima kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji wa masomo yanayofaa kufundishwa kwa Kiingereza darasani. Mahojiano haya yalichukua dakika 45. Mahojiano yalifanywa katika darasa maalumu ambalo halikuwa na kelele yoyote. Kwa hivyo mazingira ya mahojiano yalikuwa mwafaka na kwa namna hii ikafanikisha ukusanyaji wa data ipasavyo.

Pia, mahojiano yalilenga kuzua majibu kuhusu sababu za kutumia Kiswahili katika vipindi vya masomo yanayofaa kufunzwa kwa Kiingereza kulingana na sera ya elimu ya lugha nchini Kenya. Mahojiano haya yalifanywa mara mbili mwanzoni na mwishoni mwa kipindi cha utafiti nyanjani. Aidha, mahojiano yalitumiwa kuyakinisha data ilikusnaywa kupitia uchunzaji darasani.

Jukumu langu katika mahojiano lilikuwa ni kuwasikiliza wanafunzi wa elimu ya watu wazima katika kaunti Turkana wakitoa maoni yao. Hata hivyo kuna wakati ambao nilionyesha hisia labda za kutoamini jambo. Kupitia mahojiano nilipata data iliyolenga maswali na malengo ya utafiti huu.

Uchunzaji

Uchunzaji ulifanywa katika gredi ya tatu na ya nne katika vipindi vya Kiingereza, hesabu na sayansi kwa muhula mzima. Mwongozo wa uchunzaji ulitumiwa kuelekeza uchunzaji. Lengo la uchunzaji ilikuwa kubaini sababu ya walimu na wanafunzi wa elimu ya watu wazima wanatumia Kiswahili katika darasa la elimu ya watu wazima. Kifaa cha kunasa za sauti pamoja kuandika matukio ilitumiwa kunakili matukio darasani.

Uchanganuzi wa Matini

Matini kuhusu tafiti mbalimbali kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo yanayofaa kufundishwa kwa Kiingereza yalichanganuliwa. Vile vile matini kuhusu elimu ya watu wazima nchini Kenya ilitathminiwa. Aidha, sera ya elimu ya lugha nchini ilichanganuliwa. Lengo la kuchanganua matini ilikuwa kubaini matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo katika darasa la elimu ya watu wazima nchini Kenya.

Watafitiwa

Watafitiwa wa utafiti huu walikuwa wanafunzi wa elimu ya watu wazima 16 kutoka kaunti ya Turkana; kiume 7 na kike 9. Walimu 4 wa darasa la elimu ya watu wazima; kiume 2 na wa kike 2. Wanafunzi wa darasa la elimu ya watu walioshiriki katika utafiti huu walikuwa kutoka kaunti ya Turkana.

MATOKEO**Kurahisisha Uelewa wa Matini**

Uchanganuzi wa data ya mahojiano na uchunzaji ilionyesha Kiswahili kinatumiwa kuwawezesha wanafunzi kuelewa matini yanayofunzwa darasani. Utafiti ulibaini kwamba wanafunzi wa ngumbaru katika kaunti ya Turkana hawaelewi lugha ya Kiingereza inayotumiwa kama lugha ya ufunzaji na ujifunzaji. Kwa hivyo walimu hulazimika kutumia Kiswahili kufundisha masomo ya Kiingereza, Sayansi, Hesabu, somo la Dini na somo la Jamii.

Kiswahili kinatumiwa kama lugha ya ufunzaji na ujifunzaji badala ya Kiingereza ambacho ni lugha ya ufunzaji na ujifunzaji nchini Kenya kulingana na sera ya lugha nchini Kenya. Matokeo haya yanawiana na tafiti zinazonyesha kwamba matumizi ya lugha ya kwanza au lugha wanafahamu wanafunzi inafanikisha wanafunzi kuelewa masomo yanayofunzwa kwa urahisi (Baker, 2006, Gracia, 2009). Zifuatazo ni kauli za wanafunzi wa darasa la elimu ya watu wazima:

“Walimu wakitumia Kiswahili tunaelewa vizuri”

“Mimi naelewa mwalimu akifundisha kwa Kiswahili”

“Mwalimu akitumia Kizungu hakuna mtu ataelewa kitu darasani”

Matokeo haya yanadhihirisha kwamba Kiswahili kinawezesha wanafunzi wa elimu ya watu wazima kuelewa masomo yanayofundishwa darasani. Hata hivyo Kiingereza pekee kinapotumiwa wanafunzi hawaelewe chochote darasani hivyo basi kukosa umilisi katika masomo yanayofundishwa kwa Kiingereza. Matokeo haya yanawiana na utafiti wa Kiramba (2016) kuwa wanafunzi katika shule msingi katika kaunti ya Meru wanakosa kuelewa masomo yanapofundishwa kwa Kiingereza. Hata hivyo walimu wanapotumia Kiswahili wanafunzi wanaelewa somo la Hesabu na Kiswahili. Vilevile matokeo ya utafiti huu yanawiana na utafiti wa Nyimbili (2021) uliodhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya kwanza yaliboresha matokeo ya wanafunzi. Pia matokeo ya utafiti huu yanawiana na tafiti zinazonyesha kuwa lugha ya kwanza hufanikisha mawasiliano katika jamii (Mwiinga na Mwanza, 2024) Aidha, utafiti wake Mwaniki (2016) ulitambua kuwa Kiswahili kinawasaidia wanafunzi kuelewa somo la Kiingereza na fasihi ya Kiingereza darasani. Tafiti hizi zinawiana na matokeo ya utafiti kuwa katika darasa la elimu ya watu wazima, Kiswahili kinatumika kuwawezesha wanafunzi kuelewa masomo ambayo

yanafundishwa darasani hivyo basi kupata umilisi darasani.

Kufanikisha Mawasiliano

Lugha ni chombo cha mawasiliano katika jamii (Habwe na wenzake, 2010; IribeMwangi na Mukhwana, 2011). Mawasiliano ni muhimu katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Mawasiliano huwawezesha wanafunzi kuelewa matini katika somo husika. Ili wanafunzi waelewe matini katika somo husika ni lazima wafahamu lugha inatumiwa katika ufunzaji na ujifunzaji. Utafiti huu ulibaini kwamba wanafunzi wa ngumburu wanafunzi hawana umilisi wa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo inakuwa vigumu kwao kuelewa matini yanayofunzwa darasani. Hii husababisha walimu wa elimu ya watu wazima kutumia Kiswahili ili kuwawezesha wanafunzi kuelewa masomo darasani. Baadhi ya kauli za wanafunzi wa darasa la elimu ya watu wazima ni:

“Mwalimu akitumia Kiswahili tupata kile kinachosema darasani”

“Sisi hutumia Kiswahili kuwasiliana darasani kwa sababu hatujui Kiingereza vizuri. Kwa hivyo tunatumia Kiswahili kuwasiliana”

“Wengi wetu hatujui Kiingereza kwa hivyo inakuwa vigumu kwetu kuwasiliana kwa Kiingereza”

Kauli hizi za wanafunzi zinadhihirisha kwamba Kiswahili kinafanikisha mawasiliano darasani. Matokeo haya yanawiana na matokeo ya Chimbutane na Lokidor (2022) kwamba Kiswahili hufanikisha mawasiliano katika kipindi cha Kiingereza katika shule za msingi katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma.

Kushirikisha Wanafunzi katika Ufunzaji na Ujifunzaji Darasani

Ilibaini kuwa walimu wanapotumia Kiswahili darasani wanafunzi wanashiriki katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji darasani. Hata hivyo walimu

wanapotumia Kiingereza kufunza masomo darasani wanafunzi hawashiriki katika ufunzaji na ujifunzaji darasani. Kwa hivyo wanafunzi hutumia Kiswahili ili kuwawezesha kushiriki katika ufunzaji na ujifunzaji darasani. Walimu wanapotumia Kiswahili, wanafunzi wanashiriki katika kipindi kwa kuuliza na kujibu maswali. Utafiti huu unawiana na tafiti zilizofanywa katika taifa ya Msumbiji ilionyesha kwamba walimu wanapotumia Kireno wanafunzi hawashiriki katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji darasani. Hata hivyo lugha ya kwanza ya wanafunzi inapotumiwa wanafunzi wanashiriki ipasavyo katika ufunzaji na ujifunzaji (Chimbutane, 2011; Chambo, 2018; Shakina, 2019). Baadhi ya wanafunzi wa darasa la elimu ya watu wazima walitoa maoni yafuatayo:

“Huwa tunatumia Kiswahili kuuliza maswali katika somo la hesabu au sayansi”

“Tunapotumia Kiswahili darasani hatuogopi kuuliza maswali kwani tunajua Kiswahili vizuri na hakuna mtu hatucheka.”

Kauli hizi za wanafunzi zinaonyesha bayana kwamba Kiswahili kinasahilisha mawasiliano darasani kwa kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika kipindi cha Hesabu au Sayansi. Hii ina maana kwamba wanafunzi wanapouliza maswali katika kipindi wanawezeshwa kuelewa masomo ya Hesabu au Sayansi. Vilevile wanafunzi hawana woga kuuliza maswali kwa Kiswahili kwa sababu hakuna mtu hatawacheka. Hali hii hupelekea wanafunzi kufanya vyema katika mtihamu kuliko wakati lugha moja wasioelewa inapotumika (Velsaco na Garcia, 2014).

“Mwalimu akiuliza swali kwa Kiswahili kila mtu anaweza kijibu. Lakini akitumia Kiingereza watu wanashindwa kujibu kwa Kiingereza”

Maoni haya yanadhihirisha kwamba matumizi ya Kiswahili yanawawezesha wanafunzi wa darasa la elimu ya watu wazima kujibu maswali darasani. Kwa namna hiyo wanafunzi wanashiriki ipasavyo katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji

darasani. Wanafunzi wanaposhiriki katika kipindi uelewe wa matini huweza kuafikiwa darasani.

“Nikitumia Kiswahili wanafunzi wanachagua darasani lakini nikitumia Kiingereza hawashiriki katika kipindi”

Kauli ya mwalimu inaonyesha kwamba Kiingereza pekee kinapotumiwa katika kipindi, kinawahini wanafunzi kushiriki katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani (Bunyi, 1999). Aidha, matokeo haya yanadhihirisha kwamba mwalimu anapotumia lugha ambayo wanafunzi wanaelewa, wanafunzi huweza kushiriki ipasavyo katika mdahalo darasani (Nambisan, 2014). Kwa hivyo Kiingereza kikitumiwa katika darasa la elimu ya watu wazima, wanafunzi hawataweza kushiriki katika kipindi kwani hawaelewi Kiingereza. Hali hii inaungwa mkono na utafiti wa Ntabo na Obiero (2017) kwamba wanafunzi katika kaunti ndogo ya Kisii Kusini wanlipendelea kutumia lugha ya kwanza kuliko Kiingereza kwa sababu hawaelewi Kiingereza.

“Tunatumia Kiswahili kuuliza mwalimu maswali iwapo hatujaelewa kitu vizuri”

Maoni haya ya wanafunzi wa elimu ya watu wazima yanadhihirisha kwamba matumizi ya Kiswahili katika darasa la elimu ya watu wazima yanawawezesha wanafunzi kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Matokeo yanawiana na utafiti wa Lokidor na Chimbutane (2022) katika kambi la Wakimbizi la Kakuma nchini Kenya, yaliyodhihirisha kwamba mwalimu anapotumia Kiswahili katika kipindi cha Kiingereza wanafunzi wanashiriki katika kipindi vizuri.

Kufanikisha Ujifunzaji Rika

Utafiti huu ulibaini kuwa Kiswahili kinawawezesha wanafunzi kujadili kazi ya makundi wanayopewa kama tamrini. Hali hii inadhihirisha kwamba Kiswahili hufanikisha ujifunzaji rika darasani na kuwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi wa masomo yanayofundishwa.

Matokeo hayo yanawiana na maoni yafuatayo ya wanafunzi wa darasa la elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana:

“Mwalimu akitupa kazi ya kufanya tunajadiliana kwa Kiswahili. Tukitumia Kiingereza hakuna mtu hatachangia katika kikundi kwani hatuelewi Kiingereza.”

“Sisi tunajadili kazi ya makundi kwa Kiswahili ingawa tutaandika majibu kwa Kiingereza.”

Kauli hii inaonyesha kwamba Kiswahili kinawawezesha wanafunzi kushiriki katika mjadala wa kazi ya makundi wanayopewa na walimu. Matokeo haya yanawiana na madai ya Gracia na Sylana (2011) kwamba lugha hufanikisha ujifunzaji kwa kuwawezesha wanafunzi kubadilishana maarifa na kuelewa matini ipasavyo.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya Kiswahili katika darasa la elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana. Utafiti huu ulibaini kwamba Kiswahili kinatumika katika ujifunzaji na ufunzaji katika darasa la elimu ya watu wazima katika kaunti ya Turkana. Ingawa kulingana na sera ya elimu ya lugha nchini Kenya, Kiingereza ndicho kinachofaa kutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo kama vile Hesabu, Kiingereza, Dini, Sayansi na Somo la jamii. Hata hivyo kutokana na ugumu wa kuelewa Kiingereza ambayo inafaa kutumiwa kufunza masomo ya haya, walimu hulazamika kutumia Kiswahili ili kuwawezesha wanafunzi kusanisi matini, kuelewa, kuwasiliana na kushiriki katika kipindi darasani. Aidha, Kiswahili kinawawezesha wanafunzi kushiriki katika ujifunzaji rika katika kazi ya makundi.

Kwa kurejelea nadharia ya Kitamaduni ya Vgotysky, lugha hutekeleza jukumu muhimu katika ufundishaji. Vile vile mwalimu huwa nafasi muhimu katika kuelekeza masomo darasani. Kwa hivyo mwalimu ulazimika kutumia Kiswahili ili kuwawezesha wanafunzi kusanisi matini, kuelewa

masomo darasani, kuwasiliana na kwa wakati uo huo kushiriki katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Utafiti huu unapendekeza Kiswahili kupewa hadhi ya lugha ya ujifunzaji na ufundishaji wa masomoni ya elimu ya watu wazima. Kwa hivyo serikali inaweza kutambua Kiswahili kama lugha ya ujifunzaji na ufundishaji masomo kutoka gredi ya kwanza hadi vyuo vikuu nchini Kenya. Vilevile utafiti huu unapendekeza utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza katika ujifunzaji na ufundishaji katika madarasa ya elimu ya watu wazima nchini Kenya. Aidha, watafiti wengine wanafunzi kufanya kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika vipindi vya masomo mengine kama Kiingereza, Hesabu, dini au historia katika shule za upili nchini Kenya.

MAREJELEO

- Baker, C. (2003). Biliteracy and transliteracy in Wales: language planning and the Welsh National Curriculum. In N. Hornberger (Ed.), *Continua of Biliteracy: An Ecological Framework for Educational Policy, Research, and Practice in Multilingual Settings* (pp.71–90). Clevedon, UK: Multilingual Matters.
- Baker, C. (2011). *Foundations of Bilingual Education and Bilingualism* (5th ed.). Clevedon, UK: Multilingual Matters.
- Bunyi, G. (1999). Rethinking the place of African Indigenous languages in African education. *International Journal of Educational Development*, 19, 337-350
- Chimbutane, F. (2011). *Rethinking Bilingual Education in Postcolonial Contexts*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Chimbutane, F. (2013). Codeswitching in L1 and L2 learning contexts: insight from a study of teachers' beliefs and practices in Mozambique bilingual education programmes. *Language and Education*, 27(4), 314–328. DOI:10.1080/09500782.2013.788022
- Chambo, G. A. (2018) *Revitalização dos Ambientes Participativos e Interactivos na Educação Bilingue em Moçambique através do Translanguaging e do Cross-Cultural Learning*. Tese de doutoramento, Universidade de Vigo (não publicada)
- Dixon, K. (2018). Access, language and structural inequality. In T. Capstick (Ed.), *Language for Resilience* (pp. 29–30). London: British Council.
- García, O. (2009). Education, multilingualism, and translanguaging in the 21st century. In T. Skutnabb-Kangas, R. Phillipson, A. Mohanty & M. Panda (Eds.), *Social Justice through Multilingual Education* (pp.140–158). Bristol, UK: Multilingual Matters.
- García, O. & Sylvan, C. (2011). Pedagogies and practices in multilingual classrooms: 113 Singularities in pluralities. *The Modern Journal*, 95(3), 385-400
- Habwe, J. na wengine (2010) *Darubini ya Isimujamii*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Iribemwangi, P.I. na Mukhwana, A. (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Kiramba, L. K. (2016). Communicative Practices in a Bi-/multilingual Rural Fourth Grade Classroom in Kenya. University of Illinois at Urbana-Champaign. (Unpublished PhD Thesis). Urbana, Illinois
- Lokidor, E.E, (2025). *Translanguaging Inside and Outside the Refugee School in Kakuma Refugee Camp in Turkana County*. Unpublished Doctoral Thesis, Faculty of Arts and Social Sciences, Maputo, Mozambique.
- Lokidor, E. E. & Chimbutane, F. (2024). Motivation for Using Translanguaging in Kakuma Refugee

Camp School *East African Journal of Education Studies*, 7(1), 201-213.
<https://doi.org/10.37284/eajes.7.1.1740>.

Nambisan, K. (2014). Teachers' attitudes towards and uses of translanguaging in English classroom in Iowa. Master's Thesis, Iowa: Iowa State University

Ntabo, K. J and Obiero, J.O (2017). Language practices and performance in English among High School Pupils of Kisii South Kenya. *Journal of Creative Practices in Language Learning and Teaching*, 5(1), 60-67

Nyimbi, F. (2021). Impact of Translanguaging as Pedagogical Practice on Literacy Learners in Luandai District, Zambia. (Unpublished PhD Thesis, The University of Zambia, Lusaka.

Mwaniki, M. (2016). Translanguaging as a class/lecture-room language management strategy in multilingual contexts: insights from autoethnographic snapshots from Kenya and South Africa. *Southern African Linguistics and Applied Language Studies*, 34(3), 197–209.

Shakina, R. (2019). *Translanguaging as Agentive and Collaborative and Socioculturally Responsive Pedagogy for Multilingual Learners*. PhD Thesis, Ontario Institute for Studies in Education. University of Toronto

Velasco, P., & García, O. (2014). Translanguaging and the writing of bilingual learners. *The Journal of the National Association for Bilingual Education*, 37(1), 6–23.